TAFITI ZA KITAIFA ZINAZOHUSU UKATILI DHIDI YA WATOTO NA VIJANA (VACS)

VACS NI NINI?

Tafiti za Kitaifa Zinazohusu Ukatili Dhidi Ya Watoto Na Vijana ("VACS", kifupisho cha Kiingereza), zinazoongozwa na Vituo vya Kimarekani Vinavyoshughulikia Udhibiti wa Magonjwa na Utoaji wa Kinga ("CDC", kifupisho cha Kiingereza) ikiwa ni sehemu ya ushirika wa Together for Girls ("TfG", kifupisho cha Kiingereza), ni tafiti za kaya zenye uwakilishi wa kitaifa zikijumuisha wavulana na wasichana wenye umri kati ya miaka 13 hadi 24.

VACS zimesanifiwa ili kupima kuenea kwa matukio na athari za ukatili wa kingono, kimwili na kisaikolojia kwa watoto, na vijana (umri chini ya miaka 18) na vijaya wakubwa zaidi (hadi miaka 24) katika kipindi cha miezi 12 iliyopita. Tafiti hizi pia zinaonyesha hatari zilizopo, kinga zilizopo na athari zitokanazo na ukatili huu.

Matokeo ya VACS huchapishwa katika ripoti za kitaifa, hutumiwa katika kuandaa mipango kasi ya kitaifa na kutoa mwongozo kwa mipango na sera madhubuti.



NI NANI ANAYETEKELEZA VACS?

Katika ngazi ya kitaifa, utekelezaji wa VACS unaongozwa na serikali kuu, kwa msaada wa kiufundi wa CDC. Utaratibu huu huziweka VACS katika muundo wa kitaifa ili kurahisisha umiliki, kujengea uwezo, na kuandaa mazingira kwa ajili ya mkakati jumuishi wa kukabiliana na ukatili baada ya upatikanaji wa taarifa kuhusu ukatili.

Kutegemeana na nchi, washirika wa TfG (kama nyongeza ya CDC) wanaweza kuwa na nafasi muhimu. Mfuko wa Umoja wa Mataifa wa Kuhudumia Watoto ("UNICEF", kifupisho cha Kiingereza) na Shirika la Kimataifa la Uhamiaji ("IOM", kifupisho cha Kiingereza) ni ya muhimu sana katika kuunga mkono nguvukazi ya sekta mbalimbali katika kuratibu tafiti hizi na jitiada za kutafuta suluisho, ili kuhakikisha ushiriki mpana na kuratibu utekelezaji kivitendo pale tafiti zinapkuwa zimekamilika. Mpango wa dharula wa raisi wa Marekani Katika Kushughulikia Tatizo la UKIMWI ("PEPFAR", kifupisho cha Kiingereza), Serikali ya Kanada, na Shirika la Marekani la Misaada ya Kimaendeleo ("USAID", kifupisho cha Kiingereza) hutoa msaada mkubwa wa kifedha na kiufundi katika utekelezaji wa VACS.

Washirika wengine kama UN Women, Shirika la Afya la Marekani Yote ("PAHO", kifupisho cha Kiingereza) na Shirika la Afya Duniani ("WHO", kifupisho cha Kiingereza) hutoa msaada muhimu wa kiufundi kwa VACS na kuhakikisha mwitikio mkubwa kwa ngazi ya nchi. Pia huwezesha kuenea zaidi kwa taarifa katika ngazi ya kanda na ngazi ya kidunia.

Matokeo na mahitimisho katika nyaraka hii ni ya waandishi wenyewe na hayawezi kuhusishwa namsimamo rasmi wa Vituo vya Kimarekani Vinavyoshughulikia Udhibiti wa Magonjwa na Utoaji wa Kinga.

JE NI TAARIFA GANI HUTOLEWA NA VACS?

VACS hutoa ushahidi wenye nguvu na uhakika juu ya ukatili wa kijinsia, kimwili na kisaikolojia kwa watoto na vijana. Dodoso lake hujumuisha maswali yahusuyo mada zifuatazo:

- **Historia (mfano: hali ya demografia, kiuchumi, kielimu)**
- **Mitazamo ya kijinsia inazohusiana na ukatili na desturi**
- **Fikra mgando juu ya usalama**
- **Kushuhudia ukatili**
- **Kuwa muanga wa ukatili**
- **Utekelezaji wa ukatili**
- **Tabia hatarishi za kiafya — ikijumuisha hatari za VVU**
- **Matokeo ya kiafya–ikijumuisha afya ya kimwili, kiakili, ujinsia na uzazi (mfano: mimba zisizotarajiwa)**
- **Utafutaji na utumiaji wa huduma baada ya kutokea ukatili**

JE ZIPI NI HATUA ZA UTEKELEZAJI WA VACS?

USANIFU WA UTAFITI: Tafiti hujumuisha sampuli iliyochaguliwa bila mpangilio yenye vijana wa umri kuanzia miaka 13-24, ikikadiria ukatili katika makundi ya kiumri, kijinsi na vigezo vingine vya kidemografia.Taarifa zote hukusanywa kupitia mahojiano ya ana kwa ana na mhojiwa kupitia wahojaji waliofunzwa vyema.

MSAADA NA HUDUMA KWA WASHIRIKI: Kutokana na asili ya ukakasi wa maswali yaliyo katika tafiti hizi, na uwezekano wa majibu yenye hisia kali ya mhojiwa au hatari zilizopo, nchi zote huandaa mpango wa rufaa na orodha ya rasilimali vinavyowezesha wahojaji kuwaunganisha washiriki na msaada pamoja na huduma husika.

MAPITIO YA KIMAADILI: VACS hufuata taratibu za kimaadili na kiusalama za kimataifa — zenye ngazi mbili za mapitio ya kimaadili: Bodi ya Mapitio ya Kitaasisi ya Vituo vya Kimarekani Vinavyoshughulikia Udhibiti wa Magonjwa na Utoaji wa Kinga na bodi za maadili za ndani ya nchi.

UKUSANYAJI WA TAARIFA: Ukusanyaji wa taarifa kupitia VACS huchukua wastani wa wiki 4 — 6 katika kila nchi. Wanaume huoji wanaume wenzao na wanawake huoji wanawake wenzao.

TAARIFA ZA VACS HUFIKIWAJE?

Ufikiwaji wa taarifa na umma unaweza kutoa fursa kwa watafiti kupanua wigo wa matumizi ya taarifa hizo. Taarifa nyingi zitokazo na VACS huwekwa hadharani kwa matumizi ya umma — ndani ya takriban mwaka mmoja baada ya kuzinduliwa kwa ripori ya utafiti huo. Upatikanaji wa taarifa hizo kwa umma huratibiwa kupitia Together for Girls na kupatikana kwa kibali maalum toka serikali za nchi husika.

KUPATA TAARIFA ZA VACS, TEMBELEA: togetherforgirls.org

KWA TAARIFA ZAIDI KUHUSU VACS, TEMBELEA:
cdc.gov/violenceprevention/childabuseandneglect/vacs/index.html